Taarifa kwa vyombo vya habari
28 Aprili 2015

Uhalifu na vurugu wa makundi ya vijana kuelekea uchaguzi huathiri wananchi

Lakini polisi na mfumo wa sheria vinaonekana kutowahudumia ipasavyo wananchi

28 Aprili, 2015, Dar es Salaam: Wananchi watatu kati ya kumi (30%) wameshakukumbana na wizi ndani ya kipindi cha mwaka jana. Kwa ujumla, nusu ya Watanzania wote wamewahi kuibiwa.

Ailimia 84 ya wananchi wanaamini kuwa kuna uwezekano wa wao kuathiriwa na makundi ya vijana wahalifu kama *Panya Road*. Mwezi Januari 2015, *Panya Road* ilileta wasiwasi mkubwa jijini Dar es Salaam kwa kufanya vitendo vya uhalifu na vurugu, tukio hili lilitawala mijadala kwenye mitandao ya kijamii na kupelekea mamia ya vijana hao kukamatwa. Wananchi sita kati ya kumi (60%) kitaifa wamewahi kusikia kuhusu *Panya Road* lakini karibu wananchi tisa kati ya kumi (87%) walisema hakuna kikundi kama hicho katika maeneo yao.

Wananchi wawili kati ya kumi (18%) wameripoti kuwa walishuhudia ghasia wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi Desemba 2014.

Matokeo haya yametolewa na Twaweza kwenye muhtasari wake wa utafiti wenye jina la *Usalama Wetu*? *Maoni ya wananchi juu ya usalama na haki*. Muhtasari huu umetokana na takwimu za *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika mara kwa mara kwa njia ya simu ya mkononi. Takwimu hizi zilikusanywa kwa wahojiwa 1,401 kutoka Tanzania Bara (Zanzibar haimo katika matokeo haya) mwezi Februari na Machi 2015.

Licha ya kuongezeka kwa matukio ya vurugu za kisiasa pamoja na wizi na hofu juu ya makundi ya vijana wahalifu, wananchi nane kati ya kumi (79%) walisema hawajawahi kabisa, au wamewahi mara chache kujihisi kutokuwa salama katika jamii zao na maeneo wanayoishi.

Hata hivyo, wananchi wanaamini kuwa mfumo wa sheria haufanyi kazi ipasavyo. Zaidi ya nusu ya wananchi (53%) wanaamini kuwa mwananchi wa kawaida ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria akitenda kosa. Lakini kuadhibiwa kwa watu wenye kipato cha chini ni vigumu sana. Wananchi wachache (14%) wanaamini kuwa watu wenye kipato cha juu wanaweza kuadhibiwa iwapo wanavunja sheria, na wengine (21%) wanaona hili pia linawezekana kwa watumishi wa umma. Idadi hii imeshuka ukilinganisha na takwimu za mwaka 2013 ambapo asilimia 39 ya wananchi walidhani kuwa watumishi wa umma watakumbana na mkono wa sheria wanapotenda makosa. Pamoja na haya yote, wananchi sita kati ya kumi (60%) wanaamini jeshi la polisi linawahudumia zaidi watu wenye pesa kuliko watanzania wa kipato cha chini.

Licha ya kuwa na imani kwamba polisi wanapendelea matajiri, wananchi wanne kati ya kumi (37%) waliripoti kwenda polisi wanapokumbana na uhalifu. Idadi hiyo hiyo (32%), wanategemea vikundi vya ulinzi vya kijamii au kamati zao za kijiji/mtaa. Baadhi hawaendi kutoa taarifa polisi kwasababu ya rushwa (29%), na wengine kwasababu polisi hawatawajali (14%). Inaonekana kwamba matukio ya ukatili dhidi

ya polisi yameongezeka. Wananchi wawili kati ya kumi (21%) wameyasikia matukio ya aina hii. Mwaka jana (2013) ni mwananchi mmoja tu kati ya kumi aliyeyasikia matukio kama haya.

Kutokana na imani ndogo na jeshi la polisi kama wanavyoripoti wananchi, watu wengi wameanzisha vikundi vya usalama vya kijamii ambavyo husimamia utekelezaji wa sheria za kawaida. Taarifa nyingi za uhalifu na vurugu zinapelekwa huko, huku wananchi watatu kati ya kumi (29%) wakiripoti kuwahi kusikia matukio ya vitisho, watu kupigwa na vikundi hivi vya usalama.

Elvis Mushi, Meneja wa *Sauti za Wananchi* alisema *"Wananchi wanakabiliwa na wizi, hofu ya magenge na kukosekana kwa usalama ifikapo kipindi cha uchaguzi. Pia wanahisi kwamba vyombo vya sheria vinaupendeleo. Hii ni changamoto kwa watunga serikali. "*

Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza, aliongeza kwa kusema *" Kwanza, wananchi wengi wanajihisi kuwa salama katika maeneo yao lakini bado wanakumbana na vitendo vya wizi, wanaogopa kuvamiwa na vikundi kama Panya Road na baadhi yao kushuhudia ghasia na vurugu za kisiasa. Aidha, wananchi wameshuhudia ongezeko la ukatili dhidi ya vituo vya polisi ndani ya miaka miwili iliyopita, jambo hili linapunguza imani yao na vyombo vya usalama. Usalama una umuhimu wa kipekee katika masuala ya kijamii na kiuchumi. Rai yetu ni kwa serikali kuyazingatia maoni haya ya wananchi katika utekelezaji wa jukumu lake la kuwahakikishia wananchi usalama wa hali na mali."*

----Mwisho----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Risha Chande
Mshauri Mwandamizi wa Mawasiliano, Twaweza
Baruapepe: rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 657 559

Ujumbe kwa wahariri

- Muhtasari huu na takwimu zilizomo vinaweza kupatikana kwenye www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza inafanya kazi kuwezesha watoto kujifunza, wananchi kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko na serikali kuwa wazi zaidi na sikivu katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Tuna programu, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na utaratibu unaoheshimika kimataifa wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu muhimu ni pamoja na *Uwezo*, tathmini kubwa ya kila mwaka ya wananchi barani Afrika inayopima viwango vya watoto vya kujifunza kwenye maelfu ya kaya, na *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu ya mkononi. Pia tunashiriki kwenye masuala ya umma na sera, kupitia ubia wetu na vyombo vya habari, juhudi za kimataifa zinazoshughulikia masuala ya uongozi kama vile mpango wa Ushirikiano na Serikali wazi (OGP).

- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza
  Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitt a** @Twaweza_NiSisi